



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 FEBRUARI, 2025

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi, pwani ya kusini, kanda ya kati na maeneo ya kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii ilichangia katika kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani ya nchi yetu.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wa Pwani ya kusini, magharibi mwa nchi, kanda ya kati, kusini na ukanda wa ziwa victoria.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 FEBRUARI, 2025

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 FEBRUARI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi, kanda ya kati na kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la kaskazini magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Pwani ya Somalia) linatarajiwa kuwa la chini kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupelekea upepo mkavu kutoka kaskazini mashariki kuelekea maeneo ya nyanda za juu kaskazini masharini na maeneo ya ukanda wa pwani na hivyo kudhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 FEBRUARI, 2025

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):

Vpindi vya Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Hali ya

ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es

Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Mvua zinazoambatana na

ngurumo za radi zinatarajiwa katika katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Vpindi vya Mvua zinazoambatana na ngurumo

za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):

Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Mvua

zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz